



SWIS-H
STATEWIDE INFANT
SCREENING - HEARING



KWA NINI MTOTO WANGU ANAHITAJI UCHUNGUZI WA KUSIKIA?

Mtoto wako atatolewa mfululizo wa uchunguzi wa afya katika wiki chache za kwanza za maisha yake. Mmojawapo ya huu ni uchunguzi wa kupoteza uwezo wa kusikia. Uchunguzi wa kusikia utatolewa haraka iwezekanavyo baada ya kuzaliwa.

Ikiwa haiwezekani kupimwa wakati wewe na mtoto wako mpo hospitalini, utatolewa uchunguzi wa kusikia kwa mtoto wako kama mgonjwa wa nje au katika mahali pa jamii pa eneo, karibu baada ya kuruhusiwa kutoka hospitali.

KWA NINI MTOTO WANGU ANAHITAJI UCHUNGUZI WA KUSIKIA?

Wastani wa mtoto mmoja au watoto wawili katika kila watoto 1000 wanaozaliwa watapata kupoteza uwezo wa kusikia wa maana.

Ni muhimu kugundua haraka iwezekanavyo jinsi mtoto wako anavyoweza kusikia ili wewe na mtoto wako muweze kupata ushauri sahihi na msaada. Wakati watoto wanaposema neno la kwanza wamekuwa wanasikiliza jinsi tunavyosema kwa wastani wa mwaka mmoja.

UCHUNGUZI WA MTOTO WANGU UNAHUSU NINI?

Mpimaji mwenye mafunzo ya kusikia atampima mtoto wako wakati amelala au ametulia. Unakaribishwa kukaa na mtoto wako wakati wa uchunguzi unapofanyika.

Mpimaji ataweka vitu vidogo vyororo vyenye fahamu kwenye kichwa cha mtoto wako na atacheza sauti nyororo yenye mwaliko itakayoingia kwenye masikio ya mtoto kupita chombo cha kusikilizia. Vitu hivi vyororo hurekodi majibu ya mtoto wako kwa sauti.

Uchunguzi kawaida hausumbui mtoto. Vipimo vinaweza kuchukua muda wa dakika 10-20 ili kumaliza.

MATOKEO

Punde tu uchunguzi wa kusikia unapomalizika, matokeo yataelezwa kwako na kuandikiwa katika Kumbukumbu ya Afya Kibinafsi (Kitabu cha Bluu).

Ikiwa matokeo yanaonyesha kwamba kunahitajika kurudiwa kupimwa tena, si lazima imaanishe kuwa mtoto wako amepoteza uwezo wake wa kusikia. Inawezekana kuna sababu zingine kwa tokeo hilo. Sababu ya kawaida sana kuhitaji kurudia kupima tena ni ugiligili (majimaji) au hali ya kuzuia katika sikio la mtoto wako baada ya kuzaliwa.

NAHITAJI KUFANYA NINI MTOTO WANGU ANAPOKUA MKUBWA ZAIDI?

Kusikia kunaweza kutoendelea sawasawa wakati ukipita.

Ni muhimu kufuatia maendeleo ya matamshi na lugha ya mtoto wako pamoja na majibu yao ya sauti.

Unaweza kutumia orodha ya kukagulia upande wa nyuma ya karatasi ili kufuatilia maendeleo ya mtoto wako.

Ukiwa unahangaika kusikia au maendeleo ya matamshi na lugha ya mtoto wako baadaye, tafadhali fanya mpango wa kupima kusikia kwa mtoto wako. Omba daktari wako wa familia kukupendekeza kwa huduma inayofaa ili kupima kusikia kwa mtoto wako.

Kusikia kunaweza kupimwa kwa umri wowote.

KWA MAELEZO ZAIDI TAFADHALI UANGALIE TOVUTI IPO CHINI:

<http://www.health.nsw.gov.au/kids-families>

Habari za miadi/wasiliano wa eneo

Kwa ushauri wa afya wasiliana na *healthdirect Australia*
<http://www.healthdirect.gov.au/>
1800 022 222



ORODHA YA KUKAGULIWA KWA KUSIKIA

Kuzaliwa mpaka miezi 3	Huvutiwa na sauti kubwa
	Hunyamaza akisikia sauti alizozoea
	Hufanya sauti za kulia polepole kama njiwa
	Huvutiwa na kusema kwa kuangalia uso wa msemaji
Miezi 3-6	Hugeuza macho au kichwa kuelekea upande wa sauti
	Huanza kufanya sauti zinazoiga kusema
	Hucheka na anafanya sauti kuonyesha jinsi anavyojihisi
Miezi 6-9	Huropokwa 'dada', 'ma-ma''baba'
	Hupiga kelele/sauti ili kuvuta macho
	Hujibu mara nyingi kwa 'hapana' na jina lake lenyewe
	Huvutiwa na kuimba na muziki
Miezi 9-12	Huiga sauti ya kusema ya wengine
	Huelewa maneno ya rahisi, km 'mpira''mbwa''baba'
	Hugeuza kichwa na kukielekeza kwa sauti nyororo
	Husema maneno ya kwanza
Miezi 12-18	Inaonekana anafahamu maneno mapya zaidi kila wiki
	Hufuata maelekezo ya rahisi ya kusema, km 'leta mpira'
	Huonyesha kuelekea watu, viungo vya mwili au vitu akiulizwa
	Huendelea kujifunza maneno mapya ya kusema ingawa labda si wazi
Miezi 18-24	Huna kati ya maeneo 100-200 anayetumia kila mara
	Husikiliza hadithi na nyimbo rahisi
	Huunganisha maneno mawili au zaidi kuwa kifungu kifupi km 'jusi zaidi'

Ukumbusho:

